

UZINDUZI WA UWEKAJI WA VIBAO VYA ANUANI ZA MAKAZI KATIKA KATA YA LUGELELE WILAYA YA MBARALI ILIYOFANYIKA TAREHE 5/4/2022

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali Mh. Reuben Mfune leo tarehe 5/4/2022 amezindua uwekaji wa vibao vya namba katika makazi ya wananchi wa mtaa cha Relini kata ya Lugelele wilaya ya Mbarali katika zoezi la Anuani za makazi

Mh. Mfune amewapongeza wananchi wa mtaa huo kwa ubunifu wao walioutumia kwa kutengeneza vibao vya namba za nyumba zao wenyewe kwa kuongozwa na mwenyekiti wa mtaa huo ndugu Peter Anania Chuma.

Mtaa wa Relini unakaya zipatazo sitini (60) ambazo kati ya hizo hadi leo kaya 32 zimewekewa vibao vya anuani za Makazi, ikiwa ni Pamoja na nyumba ambazo zinaendelea na ujenzi.

Pia Mkuu wa wilaya ameagiza Ndani ya wiki moja wahakikishe kaya zote ambazo hazina vibao vya namba zinawekewa ili kukamilisha zoezi hilo katika mtaa wa Relini kama wananchi walivyomuahidi.

Pia Mkuu wa wilaya amemuagiza Mratibu wa zoezi la anuani za makazi ndugu Geoffrey Mwaijobele na Mh. Diwani wa kata hiyo Ndugu Stephano Lusulo kusimamia zoezi hili kwa mitaa iliyobaki ndani ya kata ya Lugelele kuhakikisha nako wanaweka vibao vya namba kama ilivyo katika mtaa huo.

Pia mh. Mkuu wa Wilaya ameagiza kata zote kuiga mfano huu wa kata ya Lugelele na lhahi ya uhamasishaji na uwekaji wa vibao vya namba katika makazi yao ili kuendana na malengo ya Serikali ya awamu ya sita ya kila kaya kuwa na anuani yake ya Makazi.